



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHU



Unapojibu tafadhali taja:  
HW/F.10/52/45

24/10/2024

## TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi anawatangazia watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kuwa, Ofisi imepokea mgao wa fedha za mikopo kwa Watumishi kwa Umma, kutoka kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha.


Aidha, watumishi wote wenye sifa za kupata mikopo mnatangaziwa kuomba mkopo huo wenye masharti nafuu kwa kuzingatia sifa zifuatazo:

- i. Awe hana mkopo unatolewa na Serikali kuu au Hazina
- ii. Mshahara wake lazima ubakiwe na 1/3 baada ya makato yote.
- iii. Mkopo anaomba haununui madeni ya mkopo ya Taasisi nyingine.
- iv. Awe tayari kukubali makato yafanyike kupitia mshahara wake ili kurejesha kiasi chote cha mkopo atakachopatiwa
- v. Mtumishi anayetaka kukopa ni lazima awe amethibitishwa kazini na ajira yake iwe katika masharti ya kudumu na pensheni.
- vi. Mkopo utakaotolewa kwa mwombaji utakatwa 4% ya mkopo mzima ikiwa 1% kwa ajili ya Bima na 3% ni riba ya mkopo.

Hivyo, watumishi wenye sifa tajwa hapo juu wanatakiwa kuandika barua za kuomba mkopo zikiambatishwa na Hati za malipo ya mishahara (salary Slip) za Mwezi wa tisa (tisa) 2024 na kuziwasilisha Idara ya Utumishi na Utawala makao makuu ya Wilaya ya Bahi.

Aidha watakaofanikiwa kupata mkopo huu wataitwa Makao Makuu ya Halmashauri kwa ajili ya kupatiwa utaratibu wa kuomba mkopo huu kupitia mfumo wa als.

Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 05/11/2024 siku ya Ijumaa saa 9:30 jioni

  
Zaina M Mfaume

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**